PRIMARY END TERM 3 EXAMS
2016

KISWAHILI
STD 7

,
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

DARASA LA SABA

KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Mara nyingi vijana hupenda mambo makubwa ____1____ yale waliyo nayo. Hupenda kutofungwa ____2____ sheria yoyote ili wapate kufanya mambo jinsi ____3____. Lakini hivi sivyo. Mtoto ____4____ kutii kanuni za nyumbani ____5____. Mtoto lazima ____6____ baba na mama kwa adabu. Lazima afundishwe utu na ____7____. Na chini ya maelekezo kama haya mtoto hawezi kusema kuwa amenyimwa uhuru! Sharti itambulike kuwa darasa la kwanza la mtoto ni nyumbani; la pili shuleni na la tatu katika maisha. Mzazi mwema hupenda ____8____ mtoto wake ____9____ na adabu ili kuimarisha jina lake.

1.	A. dhidi ya	B. mbali na	C. zaidi ya	D. kando ya
2.	A. na	B. kwa	C. katika	D. kwenye
3.	A. wapendapo	B. wapendavyo	C. wapendao	D. wapendacho
4.	A. ana budi	B. hiari	C. si budi	D. hana budi
5.	A. ,	B. .	C. ;	D. :
6.	A. amkabili	B. akabili	C. akabidhi	D. amkabidhi
7.	A. kaitambwa	B. kumtambua	C. kuutambua	D. kuwatambua
8.	A. kumuona	B. kumwona	C. kuwaona	D. kuona
9.	A. akiwa	B. akikuwa	C. akikuuwa	D. akikua

Shirika ____10____ maendeleo la umoja wa mataifa ____11____ na mtazamo wa katibu wa umoja mwenyewe. Kimsingi tunajifungamanisha katika msingi kwamba maendeleo ____12____ kuwapo bila ya ____13____ na usalama ____14____ watu na kwamba umoja wa mataifa lazima iwe msukumo wa maendeleo ____15____ amani.

10.	A. la	B. ya	C. wa	D. za
11.	A. linafikana	B. linaafikana	C. linaafikiana	D. yanaafikiana
12.	A. haiezi	B. hauwezi	C. haiwezi	D. hayawezi
13.	A. imani	B. amini	C. amani	D. amina
14.	A. wa	B. ya	C. kuwa	D. za
15.	A. wa	B. na	C. ya	D. kwa

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo

16. Chagua sentensi iliyo sahihi.
A. Mchezaji ambaye alituzwa ni mjasiri.
B. Mchezaji ambaye aliyotuzwa ni jasiri
C. Mchezaji ambaye alituzwa ni jasiri
D. Mchezaji ambaye aliyetuzwa ni jasiri

17. Ni sentensi ipi inayoonyesha hali ya kutendewa?
A. Mwakio aliendesha gari kwa kasi.
B. Mwalimu Majisifu anafunza somo la Kiswahili.
C. Obierika aliandikiwa waraka na mjukuu wake.
D. Tembo ananavya babake.

18. Ni orodha ipi yenye msamiati wa nasaba pekee?
A. Umbu, upwa, msusi, mkoi
B. Binamu, mbiomba, hale, hau
C. Mpwa, shemeji, wifi, mwali
D. Mbiomba, hale, hau, katibu

19. *Sentensi* Kabatini ambalo nilitia vitabu mlifungwa ina kosa. Irekebishe.
A. Kabatini ambako nilitia vitabu mlifungwa.
B. Kabatini ambapo nilitia vitabu mlifungwa
C. Kabatini ambamo nilitia vitabu mlifungwa
D. Kabatini ambayo nilitia vitabu mlifungwa

20. Ni sentensi ipi inayotumia kwa kuonyesha kusudi?
A. Waliandamana moja kwa moja hadi nyumbani.
B. Kuimba kwao kunwafurahisha wengi.
C. Wageni wataandaliwa wali kwa kitoweo cha kuku.
D. Aliadhibiwa kwa kukosa adabu.

21. Tambua sentensi iliyo na kivumishi cha pekee chenye maana ya kutobagua.
A. Uwanja wowote utafaa kwa mchezo huo
B. Sisi sote tuliabiri gari hilo
C. Ungwana wao uliwapa sifa kenyekenye
D. Waraka mwingine umeandikwa

22. *Jaza nafasi kwa kivumishi kiashiria radidi kifaacho.*
Kiatu _____ ndicho kilichonunuliwa jana.
A. kicho hicho
B. hicho hicho
C. hiki kiki
D. chicho hicho

23. Kisawe cha neno kipindupindu ni
A. ukoma B. tetewanga
C. malale D. waba

24. Taja jina la umbo hili

A. Hori B. Geli
C. Kopa D. Tao

25. Andika 111.01% kwa maneno.
A. Moja mia na moja nukta sufuri moja
B. Asili mia moja na kumi na moja nukta sufuri moja
C. Asilimia mia moja kumi na moja nukta sufuri moja
D. Asilimia moja na kumi na moja

26. *Tambua ukubwa wa sentensi hii:*
Nyumba ya ndege huitwa kiota.
A. Jumba la ndege huitwa jiota.
B. Chumba cha kidege huitwa kijiota.
C. Nyumba za ndege huitwa viota.
D. Majumba ya madege huitwa majiota.

27. *Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.*
A. Ephy alinunua: kalamu, kifutio, na kitabu
B. Ephy alinunua, kalamu, kifutio na kitabu
C. Ephy alinunua: kalamu, kifutio na kitabu
D. Ephy alinunua; kalamu kifutio na kitabu

28. Majira ya mvua ndogo ndogo kati ya Julai na Oktoba huitwa
A. matlai B. mchoo
C. yahoni D. vuli

29. *Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi.*
Mkate huu _____ mtamu kama ule.
A. si B. siyo
C. siwo D. sio

30. Tambua methali iliyo tofauti na nyingine
A. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti
B. Penye urembo ndipo penye urimbo
C. Yote yang'aayo si dhababu
D. Atanganaye sana na jua hujua

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.

Katika shule za msingi mwanafunzi wa darasa la nane yaani **mtahiniwa** anapaswa kuwa anazielewa nje ndani Insha zifuatazo kabla hajaufanya mtihani wake wa kitaifa. Insha ya barua, Insha ya maelezo, Insha ya mdokezo, Insha ya hotuba, Insha ya mjadala, Insha ya mazungumzo, Insha ya kumbukumbu, Insha ya methali na Insha za picha.

Insha za wasifu ni zile zinazotoa maelezo kueleza sifa za mtu, mahali au kitu. Insha hizi hutoa picha kamili kuhusu kinachosimuliwa. Insha za barua; iwe rasmi au kirafiki ni maandishi yenye ujumbe unaopelekwa kwa mtu mwingine kwa njia ya mkono, posta au kupita kwa tarakilishi.

Isitoshe, Insha ya maelezo hutoa habari juu ya mambo, kitu, kitendo, tabia, maumbile au tukio la jambo fulani. Insha za masimulizi ni maelezo ya kisa au tukio fulani. Tukio hili linaweza kuwa la ukweli au la kubuni. Insha ya hotuba ni maelezo maalum yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya watu. Anayetoa hotuba huitwa hatibu, wasikilizaji wake ni hadhira.

Fauka ya hayo, Insha ya mjadala ni ya kutoa hoja kuunga au kupinga mada fulani. Pia huitwa Insha ya mdahalo. Insha ya mazungumzo ni ile watu huwasiliana kwa maongezi. Maongezi haya huhusisha

watu wawili au zaidi. Insha ya kumbukumbu ni ya rekodi ya taarifa ya mkutano rasmi. Ilhali ya mdokezo ni pale mwanafunzi hupewa muhtasari wa kisa halafu anahitajika kukiendeleza. Insha hizi zinaweza kuwa za kumalizia, zenye kichwa au zenye kianzio. Insha ya methali hulenga kueleza kisa kinachooana na methali uliyopewa. Mwanafunzi lazima ajue maana ya nje na ndani ya methali husika. Insha ya picha, mwanafunzi hupewa picha ambazo anapaswa kuziangalia kwa makini kisha anaifasiri kwa njia yake kulingana na taswira anayoipata.

Mwanafunzi anapoandika Insha, mtahini husahihisha naye huangalia maudhui, msamiati, mtindo wa mpango, sarufi na mtiririko wa Insha. Maudhui huwa ni alama ishirini, msamiati ni alama kumi na mbili. Vipengele hivi viwili ndivyo vinavyokuwa na alama nyingi.

31. Mwanafunzi wa shule ya msingi anapaswa kuwa ametalii Insha zifuatazo ila
A. Insha za ripoti
B. Insha za methali
C. Insha za kumbukumbu
D. Insha za mdahalo

32. "...mtahiniwa" maana yake ni
A. anayesahihisha mtihani
B. anayefanya mtihani
C. anayetunga mtihani
D. anayeandika Insha

33. **"Isitoshe, fauka ya hayo...."** Haya ni aina gani ya mancno kama yalivyotumika katika taarifa?
A. viunganishi B. vihusishi
C. vivumishi D. vielezi

34. Mtahini anaposahihisha Insha huangalia mambo yafuatayo ila moja kabla hajatoa alama zake. Gani?
A. Methali na mapambo ya Insha
B. Mtindo wa Insha
C. Upachizi wa msamiati
D. Mambo muhimu katika Insha

35. Tofauti kati ya barua rasmi na ya kirafiki ni ipi?
A. Barua ya kirafiki ni ya ofisi ilhali rasmi ni ya ndugu kwa jamaa
B. Barua rasmi ni kwa jamaa ilhali ya kirafiki ni ya jamii
C. Barua ya kirafiki haitiwi saini ilhali rasmi huwekwa sahihi
D. Hakuna tofauti kwani zote ni barua tu

36. Ni Insha gani inapaswa kuifasiri kabla ya kuandika?
A. Insha ya methali B. Insha za picha
C. Insha za mjadala D. Insha zote

37. Kulingana na kifungu, msamiati ni nini?
A. Mapambo katika Insha
B. Maneno magumu katika Insha
C. Jumla ya maneno husika katika Insha
D. Misemo ya Kiswahili

38. Kulingana na taarifa hii mtahini
A. hutoa alama zake kwa kufuata vipengele maalum
B. ni anayeandika Insha katika mtihani
C. mwanafunzi hodari kwa Insha
D. hutoa alama kwa kukadiria tu

39. Mpangilio bora wa matukio katika Insha ni upi kulingana na wewe?
A. Utangulizi, mwili, hitimisho
B. Mwanzo, tamati na mwili
C. Hitimisho, utangulizi na mapambo
D. Maudhui, msamiati na hitimisho

40. Kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea taarifa hii ni
A. Aina za Insha
B. Mwanafunzi wa shule ya msingi
C. Mifano ya Insha
D. Mambo anayoangalia mtahini

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.

Muhula wa kwanza ulikuwa wakati alioufurahia sana Roba. Alikuwa namba tatu kati ya wanafunzi arubaini wa kidato cha kwanza. Mwalimu wake wa darasa alimpongeza sana kwa kuwashinda wenzake waliomshinda kwa maksi walipokuwa katika shule ya msingi.

Nyumbani alifika salama. Alieleza mengi kuhusu shule yake mpya. Waliposikia namba aliyokuwa wote walimhimiza kuendelea kujitahidi masomoni.

Likizo yake iliendelea vyema. Aliwasaidia wavyele wake kufanya shughuli kama kuteka maji, kurembesha ua na mengine. Hakusahau kutenga wakati wa kusoma. Alijua elimu huangaza.

Siku moja Roba aliandamana na kijana jirani yao kwenda kujionea mashindano ya michezo ya kuigiza katika ukumbi wa jamii katika lokesheni yao. Waigizaji walionyesha mbwembwe zao. Maudhui

© Stepford

yalilenga kuimarisha umoja wa watu, umuhimu wa kuhifadhi utamaduni nafasi ya elimu katika jamii na kutia bidii katika kazi. Roba alipendezwa na michezo hiyo ambayo ndiyo mara yake ya kwanza kuhudhuria.

Walipokuwa wakirudi nyumbani, Dodi alimweleza rafikiye, 'Roba nipeleke pale." Roba alisita kwanza kwa kuwa alipoonyeshwa palikuwa mahali walipokusanyika vijana kama kumi hivi. Kumbe walikuwa wanacheza kamari ya pata potea!

Walimsalimu Dodi, Roba akajulishwa kwao. Mchezo ulinoga. Dodi akawa ameshinda pesa taslimu. Shilingi mia tatu. Wakaondoka. Wawili hao walienda wakanunua soda. Wakanywa baadaye wakaelekea makwao. Roba aliwahi kuelezwa kuwa mchezo hu si mzuri kushiriki. "Lakini leo nimeona mtu akishinda na kuninunulfa soda!?

Mei tarehe tano ni tarehe ambayo Roba aliandika katika kumbukumbu yake ya maisha.

Ni siku aliyoondoka kwao kuelekea shuleni tayari kuanza muhula wa pili. Alifika mjini alikojiambia ajaribu bahati yake katika mchezo ule wa pata potea. Alitia shilingi mia moja akashinda. Akaweka zote shilingi mia mbili akapata mia nane. Moyoni alifurahi sana. Akaweka pesa zake zote juu ya ubao ule ule wa kucheza akitumai kuzirufufisha. Akilini alikuwa ameshaanza kufanya bajeti ya shilingi mia nane. Huku haya yakiendelea moyoni aliomba dua ya matumaini. Akaelezwa ameshindwa au kama walivyosema wenyewe ali finywa. Roba afanye nini shilingi hizo mia moja ndizo nauli ya kuenda shuleni. Akaingiwa na kiwi, akaanguka pu! Akazirai.

Fahamu yake iliporudi, Roba alianza kutembea mjini asijue la kufanya. Gafla gari likasimama karibu naye. Mwalimu wake alitambua sare za shule yake. Walipokuwa njiani Roba alidai kuwa pesa zake zilikuwa zimechomolewa na sinzia. Alipoulizwa wapi, alisema sehemu ambayo mwalimu alihisi sivyo. "Eti karibu na jengo la makavazi ya kitaifa?" Mwalimu alishangaa kwani alikuwa mahali hapo na hakusikia kisa chochote cha wizi.

Roba akaona aseme ukweli. "Nilicheza pata potea nikafutwa. Nisamehe mwalimu. Sitarudia," wakafika shuleni.

41. Ni nini haikulengwa na uigizaji uliohudhuriwa na Roba?
A. Nafasi ya elimu katika jamii
B. Uimarishaji umoja wa watu
C. Umuhimu wa kihifadhi utamaduni
D. Umuhimu wa kuzembea kazini

42. Dodi alimweleza rafiki yake, "Roba nipeleke pale! Kwa usemi wa taarifa ni
A. "Roba nipeleke pale rafikiye alisema"
B. Dodi alimtaka rafikiye ampeleke pale
C. Roba alimtaka rafikiye ampeleke pale
D. Dodi alimtaka rafikiye amleta hapa

43. Kwa nini Mei tarehe tano ni tarehe ambayo Roba aliandika kwenye kumbukumbu yake?
A. Alishinda pesa taslimu
B. Ilikuwa siku yake ya kwanza shuleni
C. Ilikuwa siku aliofunga safari kuelekea shuleni
D. Alishinda katika mchezo wa pata potea

44. Kwa nini Roba alianza kufanya bajeti ya shilingi mia nane?
A. Alikuwa ameshinda pesa hizi zote
B. Alitazamia kupata pesa hizi zote
C. Alikuya na uhakika wa kushinda pesa hizo
D. Pesa hizi zote alizitia kibindoni

45. Kwa nini Roba alizirai?
A. Aliugua ugonjwa hatari
B. Alipata mshtuko wa moyo
C. Alishangaa alivyoshinda pesa zile
D. Alipoteza pesa zote shilingi mia nane

46. Neno kiwi kama lilivyotumika katika taarifa hii ina maana sawa na
A. Aina ya ndege fulani mkubwa
B. Rangi ya viatu
C. Genge la majambazi
D. Giza linalomtoka mtu baada ya kushtuka

47. Akaanguka pu! Ni fani gani ya lugha?
A. Tanakali ya sauti B. Tashbihi
C. Kiunganishi D. Methali

48. Kwa nini Roba alianza kutetemeka?
A. Alikuwa amezirai
B. Mwalimu aligundua uongo wake
C. Alikuwa anaugua ugonjwa hatari
D. Alishtuliwa na gari lililosimama karibu

49. "Eti karibu na jengo la makavazi ya kitaifa" Neno lililopigwa mstari lina maana sawa na
A. chumba cha kufanya uchunguzi wa kisayansi
B. chumba kinachotumika kuhifadhi vitabu
C. chumba cha kuhifadhi maiti
D. chumba cha kuhifadhi vitu vya kale

50. Kichwa kinachofaa makala haya ni
A. Siku ambayo sitaisahau
B. Roba atapeliwa
C. Roba azirai mjini
D. Maisha ya mjini